

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KONGAMANO LA UTAFITI WA KISAYANSI LA BONDE LA ZIWA VICTORIA

1. UTANGULIZI

Bonde la Ziwa Victoria lilitengwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kama eneo maalum la pamoja lenye maslahi ya ukuaji wa kiuchumi ambalo linapaswa kuendelezwa kwa pamoja na Nchi wanachama ambao wamejipanga kuhakikisha wanasimamia Itifaki ya Maendeleo Endelevu ya Bonde la Ziwa Victoria mwaka 2003. Katika Ibara ya 3 ya Itifaki, Nchi hizi zimekubaliana uendelezaji wa utafiti ili kujenga uwezo na kubadilishana taarifa mbalimbali. Aidha, itifaki hii ndiyo iliyounda Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria.

Katika kutekeleza majukumu yake, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria inatekeleza miradi mbalimbali ukiwemo Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria, ambapo kwa sasa utekelezaji wa awamu ya pili unaendelea. Mkutano wa 16 wa Baraza la Mawaziri la Kisekta la Bonde la Ziwa Victoria uliidhinisha kufanyika kwa kongamano la Utafiti wa Kisayansi.

2. KONGAMANO LA UTAFITI WA KISAYANSI LA BONDE LA ZIWA VICTORIA

Kongamano la Utafiti wa kisayansi la Bonde la Ziwa Victoria limepangwa kufanyika tarehe 15 na 16 Februari, 2017 katika hoteli ya Malaika Jijini Mwanza. Kongamano hili limeandaliwa na Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria kwa kushirikiana na Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Takribani wadau 500 wa mazingira ya Bonde la Ziwa Victoria wanatarajiwa kushiriki kutoka Nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania.

Kauli mbiu ya Kongamano hilo ni **‘kuoanisha Tafiti na Sayansi katika kuboresha Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali mtambuka za Bonde la Ziwa Victoria’**. Kauli mbiu hii itafikiwa kwa uwasilishaji wa mada mbalimbali na majadiliano.

3. DHUMUNI LA KONGAMANO

Dhumuni la kongamano ni kukutanisha wadau kutoka sekta mbalimbali zinazojihusisha na ziwa Victoria na kutoa taarifa za uzoefu wao katika kulilinda ziwa Victoria, Taarifa hizo zitakusanywa na kusambazwa kwa wadau ili zitumike katika kuboresha ziwa. Aidha madhumuni mengine ni pamoja na :

- i Kuchangia na kukusanya taarifa/elimu/ujuzi zinazohusiana na Bonde la Ziwa Victoria
- ii Kusambaza mafanikio ya Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Victoria awamu ya pili (LVEMP II) kwa wadau
- iii Kutoa fursa kwa wadau mbalimbali kukutana na kubadilishana mawazo juu ya namna bora ya kuendeleza Mradi wa Hifadhi ya Mazingira ya Ziwa.

4. SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA:

Shughuli zitakazofanyika ni pamoja na Uzinduzi rasmi wa kongamano utakaofanywa na **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, uwasilishaji wa mada mbalimbali, maonesho ya shughuli mbalimbali za LVEMP II na shughuli mbalimbali za wadau wengine. Jumla ya mada 40 zitawasilishwa katika kipindi hiki cha kongamano.

FAIDA ZA KONGAMANO KWA TAIFA

Kufanyika kwa kongamano hili kutaleta faida zifuatazo kwa taifa letu la Tanzania:

- i. Mipango/mikakati mbalimbali itaweza kuibuliwa itakayosaidia kuendeleza rasilimali za Bonde la Ziwa Victoria.
- ii. Ushiriki wa watu kutoka sehemu mbalimbali za Dunia utatuletea fedha za kigeni
- iii. Wafanya biashara wetu wataweza kufaidika na hatimaye Serikali kukusanya kodi; na
- iv. Uwekezaji kwenye Bonde la Ziwa Victoria unaweza kuongezeka baada ya wadau kushiriki na kujionea fursa mbalimbali zilizopo

WITO

Kwa niaba ya Wananchi wote wa Mkoa wa Mwanza na Serikali ya Mkoa wa Mwanza napenda kuwakaribisha wageni wote Mwanza na kuwaomba wananchi pamoja na wadau mbalimbali wa Ziwa Victoria kushiriki kikamilifu katika kongamano hilo na kutoa michango yao ya mawazo ya namna ya kuilinda rasilimali yetu hii ya Ziwa Victoria

Imetolewa na: **Mheshimiwa John V.K. Mongella,**

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza

13 Januari, 2017